

## WARAKA WA PAULO KWA FILEMONI

<sup>1</sup> Mimi Paulo, mfungwa kwa ajili ya Kristo Yesu, na ndugu Timotheo, ninakuandikia wewe Filemoni mpendwa, mfanyakazi mwenzetu <sup>2</sup> na kanisa linalokutana nyumbani kwako, na wewe dada Afia, na askari mwenzetu Arkupo. <sup>3</sup> Tunawatakieni neema na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana yesu Kristo. <sup>4</sup> Kila wakati ninaposali nakukumbuka wewe Filemoni, na kumshukuru Mungu <sup>5</sup> maana nasikia habari za imani yako kwa Bwana wetu Yesu na upendo wako kwa watu wote wa Mungu. <sup>6</sup> Naomba ili imani hiyo unayoshiriki pamoja nasi ikuwezeshe kuwa na ujuzi mkamilifu zaidi wa baraka zote tunazopata katika kuungana kwetu na Kristo. <sup>7</sup> Ndugu, upendo wako yameniletea furaha kubwa na kunipa moyo sana! Nawe umeichangamsha mioyo ya watu wa Mungu. <sup>8</sup> Kwa sababu hiyo, ningeweza, kwa uhodari kabisa, nikiwa ndugu yako katika Kristo, kukuamuru ufanye unachopaswa kufanya. <sup>9</sup> Lakini kwa sababu ya upendo, ni afadhali zaidi nikuombe. Nafanya hivi ingawa mimi ni Paulo, balozi wa Kristo Yesu, na sasa pia mfungwa kwa ajili yake. <sup>10</sup> Basi, ninalo ombi moja kwako kuhusu mwanangu Onesimo, ambaye ni mwanangu katika Kristo kwani nimekuwa baba yake nikiwa kifungoni. <sup>11</sup> Ni Onesimo yuleyule ambaye wakati mmoja alikuwa

hakufai kitu, lakini sasa ananifaa mimi na wewe pia. <sup>12</sup> Sasa namrudisha kwako, naye ni kama moyo wangu mimi mwenyewe. <sup>13</sup> Ningependa akae nami hapa anisaidie badala yako wakati niwapo kifungoni kwa sababu ya Habari Njema. <sup>14</sup> Lakini sitafanya chochote bila kibali chako. Sipendi kukulazimisha unisaidie, kwani wema wako unapaswa kutokana na hiari yako wewe mwenyewe na si kwa kulazimika. <sup>15</sup> Labda Onesimo aliondoka kwako kwa kitambo tu, kusudi uweze tena kuwa naye daima. <sup>16</sup> Na sasa yeye si mtumwa tu, ila ni bora zaidi ya mtumwa: yeye ni ndugu yetu mpenzi. Na wa maana sana kwangu mimi, na kwako atakuwa wa maana zaidi kama mtumwa na kama ndugu katika Bwana. <sup>17</sup> Basi, ikiwa wanitambua mimi kuwa mwenzako, mpokee tena kama vile ungenipokea mimi mwenyewe. <sup>18</sup> Kama alikuwa amekukosea kitu, au alikuwa na deni lako, basi, unidai mimi. <sup>19</sup> Naandika jambo hili kwa mkono wangu mwenyewe: Mimi Paulo nitalipa! (Tena sina haja ya kusema kwamba wewe unalo deni kwangu la nafsi yako.) <sup>20</sup> Haya, basi, ndugu yangu, nifanyie jambo hilo kwa ajili ya jina la Bwana; burudisha moyo wangu kama ndugu katika Kristo. <sup>21</sup> Naandika nikitumaini kwamba utanikubalia ombi langu; tena najua kwamba utafanya hata zaidi ya haya ninayokuomba. <sup>22</sup> Pamoja na hayo, nitayarishie chumba kwani natumaini kwamba kwa sala zenu, Mungu atanijalia niwatembeleeni. <sup>23</sup> Epafra, mfungwa mwenzangu kwa ajili ya Kristo Yesu, anakusalimu. <sup>24</sup> Nao akina Marko, Aristarko, Dema na Luka, wafanyakazi

wenzangu, wanakusalimu. <sup>25</sup> Nawatakieni ninyi nyote neema ya Bwana wetu Yesu Kristo.

**Biblia Takatifu**  
**Portions of the New Testament in the Swahili**  
**Language of Kenya, Mozambique, Somalia, and**  
**Tanzania, translation by Dr. Johann Ludvig Krapf**  
**completed in 1850**

Public Domain

Language: Kiswahili (Swahili)

Dialect: Kimvita

Translation by: Dr. Johann Ludvig Krapf

2014-08-25

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 22 Feb 2024 from source files  
dated 31 Aug 2023

62071dc0-70e6-5b86-b569-c1b45e7771bd